

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**

# **T A N G A Z O**

1. Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anakaribisha maombi kutoka kwa Fundi wenyewe uwezo wa kujenga Nyumba ya kuishi familia sita (six in one) katika shule ya sekondari Lituhi  
Waombaji wenyewe sifa zifuatazo wanakaribishwa;-
  - a. Awe na uelewa wa kusoma Ramani.
  - b. Awe na akaunti ya Benki.
  - c. Awe na vitendea kazi kama vile ṭoroli, chepe, pima maji, nk.
  - d. Awasilishe kazi za aina hiyo alizowahi kufanya na kusimamia
  - e. Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu.
  - f. Awe na uwezo wa kuandaa mpango kazi.
2. Maombi kwa waliokidhi sifa zilizotajwa wafike kwenye Ofisi Kitengo cha manunuzi(PMU) Katika ofisi ya Mkurugenzi mtendaji(W) Nyasa kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 jioni kuanzia tarehe 17/05/2018 – 22/05/2018 (Siku za kazi) kwa ajili ya kuchukua **fomu za maombi**. Fomu za maombi zinapatikana **bila malipo**.


**Maombi hayo yaandikwe na kutumwa kwa ;-**

**Katibu wa Bodi ya Zabuni.  
Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa  
S.L.P 90. MBAMBA BAY.**

3. Kotesheni zote ziwe na nakala mbili (original 1 na copy 1) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na. LGA/LTH-SEC/2017-2018/W/01 [HUDUMA YA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA NYUMBA YA FAMILIA SITA SHULE YA SEKONDARI LITUHI] Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya zabuni Halmashauri ya wilaya ya Nyasa.

4. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni tarehe **25- 05- 2018** kabla ya Saa tano na nusu **5.30** asubuhi. Kotesheni zitafunguliwa hadharani kuanzia Saa tano na nusu **5.30** asubuhi mbele ya waombaji/wawakilishi watakaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa Zabuni katika Ofisi za Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya wilaya ya Nyasa.
5. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kwa hali yoyote ile kotesheni hazitakubaliwa kwa tathmini.

**Maelezo zaidi yanapatikana katika fomu za maombi.**



Eng. Evaristo G. Ngole \*

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI(W)**

